

Sigillum Dei Aei Hui

Muhuri Wa Mungu Aliye Hai

Sala hii maalum ni zawadi kutoka kwa Mungu Baba aliyopewa nabii Maria Divine Mercy kwa ajili ya ulinzi wa watoto wote wa mungu. Ni ujumbe 351, alipokea Februari 20, 2012.



Wote ambao wanakubali muhuri huu mtapewa ulinzi kila mmoja wenu na familia yako kwa wakati wa kipindi kinachoongoza hadi ujio wa pili wa Kristo.

Inuka sasa na kukubali Muhuri Wangu, Muhuri wa mungu Aliye Hai. Soma sala hii ya Crusade (33) kuukiri Muhuri Wangu na kuukubali kwa furaha, upendo na shukrani.



Hi Mungu Wangu, Baba Yangu mpendwa, nakubali kwa furaha na shukrani Muhuri Wako Wa Kimungu Wa Ulinzi. Uungu wako umezunguka mwili na roho zangu milele. Nainama kwa unyenyekevu na shukrani na kutoa upendo wangu kwa kina na uaminifu kwa wewe

Baba Yangu Mpendwa. Nakuomba unilinde mimi na wapendwa wangu na Muhuri huu maalum na nadhamini huduma zako daima milele nakupenda Mpendwa Baba Yangu. Nakufariji wakati huu Mpendwa Baba Yangu. Nakukabithi mwili, damu, nafsi na uungu wa mwana wako mpendwa katika upatanisho kwa ajili ya dhambi za ulimwengu na kwa ajili ya wokovu wa watoto wako wote. Amina.

Nendeni, watoto wangu na msigope. Mnitumaini mimi, Baba Yenu Mpendwa, aliyewaumba kwa upendo. Nafahamu kila nafsi zenu, kila sehemu yako inajulikana kwangu. Hakuna hata mmoja wenu anayependwa zaidi kuliko wengine. Kwa sababu hiyo. Sitaki kupoteza nafsi moja. Hata mmoja. Tafadhali endelea kuomba huruma yangu ya kimungu kila siku. Siku moja, utaelewa kwanini utakaso huu unaitajika.

Baba Yako Mpendwa Mbinguni

Mungu Aliye Juu